




Afya ya wanaume

Ni SAWA kuongea kuhusu afya ya ngono

Mfumo wa uzazi



Tezi kibofu ni kiungo kidogo cha uzazi ambacho ni muhimu ndani mwilini

Kibofu cha mkojo ni sehemu ya mwili inayohifadhi mkojo

Mrija wa mkojo ni bomba linalopitisha mkojo kutoka kwenye kibofu cha mkojo kwa ufunguzi wa uume

Kusimika ni ugumu wa uume

Kumwaga shahawa ni ambapo shahawa (majimaji meupe) inatoka kwenye uume.

Habari kuhusu mifumo ya uzazi zinaweza kutokuwa kweli kwa wanaume wote, kwa mfano, watu ambao wanabadilisha jinsia au wanao jinsia mbili.

Baadhi ya wanaume wanaweza kuwa na majeraha au ulemavu ambao unaweza kuathiri mfumo wao wa uzazi.

Ikiwa una wasiwasi au una maswali, zungumza na daktari.

Miadi ni ya siri.

Unaweza kuomba mkalimani.

Matatizo ya tezi kibofu na ya mkojo

Matatizo ya tezi kibofu yanajumuisha:

- Tezi kibofu kuwa kubwa zaidi ambayo inaweza kuathiri uwezo wako kukojoa kwa kuwa tezi kibofu ni chini ya kibofu cha mkojo
- Maumivu na uvimbe
- Saratani ya tezi kibofu. Katika hatua za mwanzo ya saratani ya tezi kibofu kunaweza kuna hakuna alama au dalili ambayo unaweza kuona au kuhisi

Matatizo ya kukojoa ni pamoja na:

- Ugumu wa kuanza kukojoa
- Mkojo unapita polepole
- Kuhitaji kukojoa mara nyingi
- Kuhitaji kwenda chooni haraka kukojoa
- Maumivu au kuchomwa wakati wa kukojoa
- Mkojo wenye kuvuja
- Si kuondoa kibofu cha mkojo (yaani bado unahitaji kukojoa baada ya umefanya)

Daktari anaweza kujadili matatizo haya na kukusaidia kuchagua usimamiaji bora au tiba.

**Tembelea
Daktari
wako.**

**Ebu
tuzungumze
juu
yake**

Matatizo ya ngono ni ya kawaida Ebu tuzungumze juu yake

Matatizo ya ngono yanaweza kutokea kwa wanaume wa umri wote, lakini yanakuwa kawaida zaidi kwa wanaume wa umri juu ya miaka 55.

**Ingawa inaweza kuwa mada
ngumu ya kuzungumzia,
matatizo haya yanatokea
kwa wanaume wengi.**

Mahali pa kupata msaada:

Wasiliana na GP/daktari wako au
piga simu kwa **13HEALTH** kwa
13 43 25 84

www.qld.gov.au/health/contacts

Michoro hai ya afya ya kingono
na ya uzazi inapatikana kutoka:
www.health.qld.gov.au



Rasilimali hii ilifanywa kwa ushirikiano na Kikundi cha Ushauri wa Afya yenye Kujibu kwa Kitamaduni na mashauriano ya jamii.

Matatizo ya ngono ni pamoja na:

- Kushindwa kuwa au kudumisha kusimika (hiyo inaitwa shida ya kusimika)
- Kukosa hamu au hamu ya chini ya kujamiana (kama hii ni shida kwako - watu wengine wana hamu kidogo kujamiana na hiyo ni sawa)
- Kumwaga shahawa ambayo inatokea mapema sana

Matatizo ya ngono yanaweza kuwa alama ya matatizo mengine ya afya:

- Ugonjwa wa kisukari (sukari ya juu katika damu)
- Shinikizo la juu la damu
- Mafuta ya juu (mafuta katika damu)
- Shida za mishipa ya moyo
- Afya ya akili (mafadhaiko au unyogovu)

Masuala mengine ya afya unayoweza kuzungumzia na daktari wako kuhusu:

- Uwezo wa kuzaa na kupata watoto (ikiwa unataka kupata watoto na unaona ni vigumu)
- Maambukizi ya zinaa/ngono (STIs) na kujamiana kwa usalama
- Ikiwa hutaki kuzaa watoto wowote tena.

